# LILE KANISA INABIDI LIJIINUE LENYEWE KATIKA NGUVU

*Mark 11: 22 – 26*
*Yesu akajibu akamwambia, mwaminini Mungu. Amin nawaambia, yeyote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwaka, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia yatakuwa yake. Kwa sababu hiyo nawaambia, yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba manayapokea, hayo yatakuwa yenu, nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, ukiwa na neno juu ya mtu ,ili na Baba yetu wa mbinguni awasamehe na ninyi makosa yeu [lakini kama ninyi hamsamehe, wala Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu ]*

Sikiliza kile nabii wa Mungu asemacho

Nataka ninyi mlipate hili sasa, lile Kanisa inabidi lijiinue lenyewe katika Nguvu za Mungu. Ki vipi? Tumekaribia sana mwisho sasa, na naamini Kanisa liko katika hali ambayo tunaweza kulifundisha mambo ya kilindi kidogo, na kufuta sehemu hii ya kujifanya kuamini itoke na kuingia katika kitu halisi, inabidi iwe ni kitu unachojuwa.

Sasa, tunataka kuzungumzia sasa juu ya imani, na imani ziko za aina nyingi: imani kamilifu "hilo ni jambo kuu. Sasa, imani, tumeambiwa katika Biblia, " imani huja kwa kusikia." (warumi 10:17) sasa, Huwezi kuokolewa bila imani (Efes 2:8 -9) na imani ni kitu fulani inakupasa uamini na kipo hapo, ambacho ni halisi na hakuna kiwezacho kukitangaza kiko hapo kwa imani(Waebr. 11:1-6)

Sasa, imani msingi wake uko juu ya msamaha kisha ( Walawi 19:17 – 18, Mark 11: 25- 26, Matayo 6:14 – 15) na kisha kama tulivyosema. Tutaziona hasa nyakati za kimitume zikienda miongoni mwetu, hilo ndilo sote twalionea njaa. Nalo liko tuu hapo mlangoni. Tunaliona lakini tunataka kuliona zaidi ya jinsi tunavyoliona. Tunalitaka hilo litiririke kwamba liwe ni msaada kwetu , na liwatiririkie na wengine.

Kumbuka, Yesu yeye hakutumia nguvu zake kwa aijili yake mwenyewe, alizitumia kwa ajili ya wengine. Kwa sababu zilitumwa kwa ajili hiyo.
Sasa,sasa,tunaona mwanzoni wanafunzi hawakuwa na hii Imani kamilifu. Hawakuwa nayo, kwa sababu walikuwa na Kristo, wakitembea pamoja Naye. lakini kisha baadae, Kristo alikuwa ndani yao (Wakolosai 1:26 – 27). Na kwa hiyo ni vigumu basi kuwa na hii imani kamilifu bila sasa kuwa na Roho Mtakatifu; Ndiye anayeileta; Ndiye anafanya. Unasema, Mitume hawakuwa na Imani kamilifu? Hapana; kwa kuwa walikuwa na mtoto mwenye pepo wa kifafa pale wakijaribu kumtoa pepo, na wasingeweza kufanya hivyo.

Na baba yake alimuona Yesu akija, na akasema tumemleta mtoto wangu kwa wanafunzi wako, na hawakuweza kumponya. "unaona? (mate 17:14 – 20) na baadae wanafunzi walimuuliza Yesu wakisema. Kwa nini sisi hatukuweza kumponya? Na Yesu akawaambia "kwasababu ya kutokuwa na Imani, na kutokuamini. " Na kutokuamini "hiyo nisawa " na ,kutokuamini kwenu hilo…
Sasa, kumbuka, walikuwa na Nguvu, Yesu aliwapa nguvu kuwaponya wagonjwa, kufufuwa wafu, na kutoa pepo, siku chache tuu zilizopita (luka 9:1 -2 matayo 10:1) walikuwa na nguvu lakini sio ile imani ya kutumia ile nguvu. Hilo hapo Kanisa, Yule Bibi arusi leo, Roho Mtakatifu yuko hapo na ile nguvu, lakini hamna imani ya kuifanya ifanye kazi. na mnaona kile ninacho maanisha? Inachukuwa imani kuifanya itende kazi.

Hapa nina risasi ambayo nimeiweka, najua kile iwezacho fanya ikilipuka, iko kama Neno. Lakini itanipasa kuifyatua hiyo bunduki. Moto inabidi uifikie hiyo baruti , baruti ina nguvu, ila inabidi kuwa na moto wa huiwasha ilipuke. Na ni kitu kile kile, baruti iko ndani ya risasi lakini inahitaji imani kuichaji na kuitupa nje,

Hicho ndicho kinacho hitajika, imani kamilifu kuwasha baruti ya Roho Mtakatifu ambayo tunayo sasa, tangu alipokuja juu Yetu, imani kuiwasha, kuona mambo makuu, ni ku …
Ile imani, kitu fulani kinachoileta imani kwako.

Yeye**, Bwana wetu Yesu Kristo** , alikuwa na imani na nguvu, zake.Yeye alifanyaje? Yeye alisema "Siwezi kufanya chochote mimi mwenyewe, (Yoh 5:19 – 20) kwa nini? Yeye alitegemea kile Yeye alichokuwa: Yeye alitegemea ufahamu wa kile alichokuwa Yeye ni Neno. Yeye alikuwa na imani na Mungu, Yule aliyemfanya Yeye kuwa lile Neno. Yeye alikuwa Mungu lile Neno, na lilikuwa ndani Yake, na hilo lilimpa Yeye imani, kwa sababu Yeye alielewa nafasi yake. Yeye alijuwa kile alichokuwa, kwa sababu maandiko yalisema Yeye alikuwa hivyo (Luka 24: 25 – 27) Na hapa kila andiko linafungana na kuthibitisha kwamba.Yeye alikuwa hasa kile maandiko yalicho sema angekuwa, na Yeye alijitambua Yeye ni nani.

Kwa hiyo, Yeye alitumainia kile Mungu alichomfanya Yeye, na kama Yeye alifanya hivyo, nasi hatuwezi kutegemea kile Mungu alichotufanya sisi waamini? Ishara hizi zitafuata na na hao waaminio, (marko 16:17 – 18). Yeye alikuwa na imani na kile Yeye alichokuwa. Na kama wewe ni mwaminio, Una imani ya kile ulicho; wewe ni mwamini na kama una imani, na Mungu, Biblia inasema hapa. . ." ikiwa mioyo yetu inatuhukumu hapo hatuwezi kuwa na imani; lakini ikiwa mioyo yetu haituhukumu, hapo tuna imani tuna ujasiri mbele za Mungu (Yoh 3: 19.22).

Lakini ili mradi unaendelea kutenda dhambi, yasiyo sahihi, huwezi kuwa na ujasiri mbele za Mungu. Kwa kuwa unajua kwamba uko makosani, bila shaka utajiweka mwenyewe huko nyuma mwenye dhambi kwa kujitambua kuwa uko makosani. Lakini ikiwa moyo wako hauku hukumu na unajitambua kuwa ni mwaminio, na hakuna kitu chochote kati yako na Mungu, unaweza kuomba utakacho na kutambua kuwa utakipata kwa sababu ni Neno ambalo umepewa kama tuu ilivyokuwa kwa wale mitume (Yoh 14: 13).

Sasa, **kitu kile tuu uwezacho kukifanya, ni kuwa na imani ya kile ulicho, Uwe na imani ya kile Neno limesema kuwa wewe ni nani.** (1 Yoh 3:14; 1Yoh 5 : 18 – 20: matayo 5:43 – 48; Galatia 4:6; Rumi 8: 16 – 17). Na Yesu alikuwa na imani juu ya Neno la Mungu lilomtambulisha kuwa Yeye alikuwa nani, "nimeandikiwa mimi"
Je Daudi katika zaburi na manabii, na wote walimuongelea Yeye? Mimi ni mkate wa Uzima ushukao toka mbinguni kwa Mungu." (Yoh 6: 48 – 51). Amina.
"Mimi ni mti ule wa Uzima toka bustani ya Eden (Mwanzo 3:24) Mimi ni hivi vyote: MIMI NIKO AMBAYE NIKO" na Yeye alijua kwa hilo, imani kamilifu, kuwa alikuwa masihi mpakwa mafuta, kwamba Roho wa Mungu alikuwa juu Yake (Luka 4: 14-21; Isaya 61: 1-3; Yoh 1:41; Yoh 4:25). Yeye alisema, sasa Mimi Mwenyewe, siwezi kufanya chochote; lakini ni Imani yangu kwa Mungu. Na **Mungu alikuwa ndani Yake . Lile Neno likidhihirishwa. Na wakati lile Neno la Mungu likija ndani yako. Linadhihirishwa, Kuwa wewe ni mwaminio. Unaona? Na mwaminio ni ile Imani ya Mungu ambayo inatenda kazi ndani yako.** Unalipenda hilo?

Napenda kufundisha hasa Imani ni nini.
Akijua Yeye ni nani, bila hata chembe ya shaka, Yeye alitambua kuwa alikuwa Mwana wa Mungu. Alilijua hilo, kwa kuwa Neno lilimtambulisha. Neno la Mungu lilimtambulisha Yeye alikuwa nani (Isaya 7:14,Isaya 9:6 – 7 ). Yeye alisema, ikiwa sitendi

kazi za Baba yangu, hapo msiniamini mimi, lakini kama ninazitenda, aminini hizo kazi, kwa **kuwa zinadhihirisha Neno lililo ahidiwa**, (zakari 9: 9 -10;Luka 19: 29 – 38; Zaburi 119: 26).Oh kama tungezinduka kwa dakika kwa ajili ya hilo. Unaona**, Neno lenyewe linamtambulisha Yeye,** alikuwa nani Na Yeye alisema nani awezaye kushuhudia kuwa mimi ni mwenye dhambi? Kwa maneno mengine, "nani awezaye kunionyesha mimi maisha yangu na kazi zangu hazitimizi hasa kile ambacho masihi angepaswa kutenda?" Hakuna aliye weza kusema kitu, kwa kile alikuwa. **Kwa hiyo alikuwa na Imani ya kuamini kwa chochote ambacho angesema kingefanyika.**

**kwa maana lile Neno lilimtambulisha, lilimtambulisha Yeye mwenyewe, alikuwa nani; na Neno lile lile linatutambulisha sisi**, unaona? " Mtu akinipenda mimi atazishika amri zangu. Ikiwa anasema ananipenda mimi, na hazishiki amri zangu (zote) yeye ni muongo; na kweli haimo ndani yake"(Yohana 14:21;1Yohana 2:3-6)

Unasema, "vema siamini zote…." Vema sasa wewe ni asiye amini; hilo tuu. Kama biblia imesema hivyo, hiyo inalifanya hilo kuwa sahihi hilo limekamilika milele. Kile Biblia imesema ni Kweli.

Sasa, unaona, Yeye alijua kuwa yeye ni nani, kwa hiyo Yeye alikuwa na Imani. Imani ingeweza kuzaa wakati Yeye alipojua kuwa Yeye ni nani. Sasa, kama mkikaa ndani yangu mimi, na Neno langu ndani yako, hapo unajua wewe ni nani
Omba utakalo utapewa wewe (Yoh 15: 7).

Yesu alikuwa na Imani kamilifu. Yeye alikuwa nayo. Na ilikuja kwa sababu Yeye alikuwa Neno. Na anakuwa Neno; wewe unakuwa lile Neno,unapo lipokea lile Neno ikiwa mtakaa ndani yangu mimi na Neno langu ndani yenu, maneno yangu (ambayo ni kitu Neno) likikaa ndani yenu, kisha ombeni mtakalo, mtatendewa ninyi. "Unaona? Na kama mkiuambia kuwa mlima ng'oka na usitilie shaka lakini waamini ulilo nena, hapo utapokea ulicho nena, uombapo amini ulichoomba utakipata, na utapewa wewe." Muda, wakati, hakuna chochote kitakacho badilisha, unajua limetendeka tayari limekwisha.

Sasa, tazama. Tazama na Yeye alituambia sisi, ikiwa mkikaa ndani yangu na maneno yangu ndani yenu, ombeni mtakalo, litatendeka. Kisha tambua nafasi yako katika maandiko kama mwaminio (1Thess 1:4:6) unaona? inakubidi utambue nafasi yako, kama Yeye alivyo tambua nafasi yake.

Lakini Yesu aliishi katika ulimwengu ambao hamna aliyeujua; Yeye alikuwa mtu wa kipekee Yeye aliishi katika ulimwengu wa Imani kamilifu katika Mungu mkamilifu, ambayo Yeye alikuwa, ikiwa tutaishi katika imani kamalifu ya Kikristo. Kwa kile tulicho, tungekuwa watu wasioeleweka kwaulimwengu: watu hawatakuwa wakikuelewa wewe ungetembea katika Roho (Wagalatia 15:16 -16) kile Yule amenena chocho utakifanya. Kile asichotaka hutakitenda, kisha watu wataanza kusema na utakuwa Mtu asieleweka kwao.

Hivyo ndivyo ilivyo kwa waamini wote, kwao ni wasio eleweka. Watu hawaelewi kwa sababu wanaishi kwenye ulimwengu wao. Yesu aliishi katika ulimwengu

ambao mtu asingeli weza kuugusa. Wale wanafunzi hawakuweza kumuelewa Yeye. Yeye aliposema nao, walisema hivi, na kisha walisema, mbona unanena kwa mafumbo(Mathayo 13:10-17) hatuelewi hili. Litakuwaje hili? Unaona? **"Hawakuwa ndani ya ule ulimwengu alimoishi Yeye,** unaona, wasingeweza kumuelewa Yeye, hakuna hata mtu mmoja alimuelewa Yeye.

Na wakati mtu anapoishi kwa Imani na kutembea kwa Imani, mimi na maanisha Imani halisi (waebrania 11:1) hutengwa na ulimwengu wote na kuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo. (11 kor 5:17) hapo, sasa unaingia katika vifaa vya Bibi Arusi. Mnaona, ona.? Unaingia katika hali ya kunyakuliwa sasa. Hiyo ina maana kwa kila mmoja wetu, sio mchungaji peke yake, shemasi, wadhamini, hiyo inamaanisha kwa mshirika, kila

mtu binafsi unatembea katika ulimwengu wewe na Mungu peke yako. Umebatizwa katika huu ufalme (I kor 12:13) na hakuna mwingine hapo ila wewe na Mungu. Unaona? Yeye hutoa maagizo, nawe unayatekeleza. Chochote asemacho Yeye, hakuna hata chembe ya shaka mahali popote unasonga mbele moja kwa moja kwa usahihi.

Ikiwa Bwana asema hiki, hakuna mtu duniani awezaye kukupeleka kinyume: unasonga mbele vile vile.

Sasa unaingia kwenye Imani kamilifu, kamilifu iliyokamilika ambayo haiwezi kushindwa. Hiyo Imani haiwezi kushindwa. Ndio, Alikuwa asiye eleweka kwao, na Imani Yake kamilifu. ndivyo ilivyo sasa kwa wale wenye Imani kamilifu, wao ni wasioeleweka kwa wengine.

Sasa, tazama, Imani kamilfu ni mtawala wa mazingira yote, Imani kamilifu huwa juu ya hali zote haijalishi ni kitu gani, yenyewe iko juu zaidi. Sasa, hebu tazama, wakati unapo amini kitu chochote na kukifanya, na una imani juu ya kile unachokielewa haijalishi kuna mazingira gani, hiyo haina uhusiano na hilo. Unaona inatawala mazingira hayo. Kama ni katika chumba cha wagonjwa, na Yeye Bwana amelifunua kwamba kitu fulani kitatendeka, wewe nena tuu na usonge mbele.

Hebu usiulize swali lolote. Kwani hilo limekwisha, wewe songa mbele, unaona? Inamiliki kila hali. "Vema, ikiwa utafanya hivyo, huyu na huyu wataenda kutenda…." unaona? Tayari imekwisha tawaliwa. Unaona.

Imani inaamini kwamba Mungu ataenda kulifanya hilo."Sijui ataenda kulifanyaje hilo Lakini Yeye ataenda kulifanya kwa vyovyote vile. Inamiliki mazingira yote.

Na Imani na upendo vinahusiana, sababu huwezi kuwa na imani hadi uwe na upendo, sababu imani yako, ni katika Mungu ambaye ndio chemchem ya Upendo. Imani na Upendo vinatenda kazi pamoja (Wagalatia 5:6)

Alinipata nilipokuwa si kitu. Bado mimi si kitu, lakini niko mikononi Mwake unaona? Yeye alinipata mimi. Na Yeye alinipenda mimi nilipokuwa sipendeki. Yeye alikupenda wewe ulipokuwa haupendeki, lakini Yeye amekubadilisha wewe.

Kama vile Yule dada mweusi, wakati ule alipotoa ushuhuda wake. Alisema. Siko ninavyopaswa kuwa, na siko ninavyotaka kuwa, na halafu siko nilivyokuwa! Yeye alitambua kuwa alitoka mahali fulani, kitu fulani kimetendeka. Na hivyo ndivyo ilivyo.

Ikiwa Mungu. Wakati nilipokuwa kinyume na Yeye, alinipenda mimi hadi Yeye alishuka chini kunifuata mimi na kuniinua. Hiyo inanipa uhakika Yeye anataka kunitumia mimi. Yeye anakusudi la kufanya hivyo Yeye aliona kitu fulani ndani yangu, aliona kitu fulani ndani yako. Yeye anasababu ya kukuokoa wewe. Tazama ni mamilioni wangapi ambao hajawachukuwa badala yako, lakini Yeye amekuchukuwa wewe. Amen. Hakuna awezaye kuchukuwa nafasi yako. Amen. Wewe uko katika mpango wa Mungu, hakuna awezaye kufanya hivyo huo ni Upendo wake kwako.

Je upendo wako hautapenda kurudi kwake Yeye na hapo kuna mapenzi, haijalishi kuna hali gani: hali yake inatawaliwa na Upendo huu ambao huumba imani; kwamba Mungu anakupenda wewe na wewe unampenda Mungu, na mnapendana mmoja kwa mwingine, na hilo kuleta imani. Vema, sasa haiwezi kuzuia kuleta kile hasa ambacho Mungu aliahidi kitatendeka. [ 1 ]

Sasa ndugu, na dada, mimi nataka kuwauliza kitu fulani.Sasa kama tumezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu …. Mungu hana sehemu ndogo dhaifu na sehemu kubwa zenye nguvu: Yeye kwa ujumla ni Mungu! na ikiwa una Mungu wa kutosha ndani yako. Hata kama ikiwa ni kivuli chake tu, hizo ni nguvu za kutosha kuumba ulimwengu mwingine. Hiyo ni nguvu ya kutosha kuumba mwezi mwingine na mfumo mpya. Ni Mungu

na ana nguvu. Na sasa hivi katika kila mwamini aliyeko hapa anao uzima wa milele, ambao ni Roho wa Mungu ndani yako; Nguvu ya kutosha ambayo inaweza kufufua wafu, ambayo inaweza kuponya wagonjwa, ambayo itaweka mfumo wa sayari mahali pake, unatawaliwa na sheria, ambayo ni Roho aliye ndani yako. Ninyi ni wana na binti za Mungu. ambaye ni Roho Yule uliye naye ndani yako, atakufufua wewe mwenyewe katika siku ile ya kufufuka.

Kama hakukuwa na sheria ya hilo, wana na Binti wa Mungu wangejiumbia ulimwengu wao nje huko na kwenda kuishi maisha yao binafsi katika huo. Una nguvu ndani yako ya kufanya hivyo (Luka 24:48 – 49; Matendo 1:8) ikiwa una kivuli cha nguvu ya Mungu ndani yako, una nguvu ya kufanya hivyo. Mungu ni mwenye uwezo wote. Unaona ninacho maanisha ? Ile nguvu iliyo ndani yake itafanya … wewe unaweza ukanena na ulimwengu ukatokea na ukaenda kuishi juu yake. Halleluyah! Hilo hapo.

Hiyo ni nguvu iliyomo Kanisani sasa (2kor 4:7-11) lakini inatawaliwa na sheria. Na sheria hiyo sio kutunza rundo la amri. Ni sheria ya Imani. Yesu alisema. " yote yawezekana kwake yeye aaminie" na kama unaweza kuamini , chchote, Mungu ataiongoza nafsi yako kuamini, uombayo yatakuwa yako.

Kwa kadiri ya Imani yako itakavyojitokeza, ndicho kiasi cha nguvu ulizo nazo, sababu ndani yako mna nguvu za kuumba mbingu na nchi, Mungu anakaa ndani yako na ninyi ni wana na binti za Mungu Amen. Uko hapo. Lakini ni Imani yako. Yesu alisema. Kulingana na Imani yako, na iwe hivyo kwako. Ikiwa unaweza kuamini, yote yawezekana ukiamini, nawaambia, ukiuambia mlima huu ng'oka, na usitilie shaka, lakini uamini uliyo yasema yatatokea, yatakuwa yako…"

Amini hili, yakupasa uamini. Tunachohitaji siku hii ya leo si kuomba kuongezewa nguvu. Una nguvu ya kutosha kuumba ulimwengu mpya (Waefeso 3:20 – 21) unachohitaji ni imani ya kuweza kutumia hiyo nguvu. Unachohitaji ni kutawala hayo maisha. [2] … sio kuwa msengenyaji, jinsi ya kutawala hasira yako, sio kughadhibika hovyo mtu yoyote anenapo kinyume nawe (2 Petro 1:3 – 14)

Kiasi. Jinsi ya kujibu kwa upole wakati umenenewa maudhi mtu fulani aseme, ninyi kundi la watakatifu wanao jivingirisha hapo chini, usiruke na kukunja mikoni ya shati sasa. Unaona? Sio hivyo, bali zungumza kwa upendo wa Mungu, kwa kiasi, upole, ni hivyo unavyotaka kuwa?

Wakati unapochukizwa, usirudishe chuki. Acha Yeye awe mfano wako!

Leo, jamani, vijana, wengi wetu twaenda kuanguka kabla hatujaanza, au sivyo? Unaona? Kisha tunashangaa kwa nini Mungu hayuko ndani ya Kanisa lake akifanya miujiza, na mambo aliyokuwa akiyafanya [ 3 ]

Ishi maisha ya kiungu, kiasi kwamba umuombapo Mungu chchote, unajua. Tunao uhakika kwa Mungu, kwa hilo. Tunajua, ikiwa tunatii amri zake Yeye, Yeye hatazuia kilichochema kwetu ikiwa tutatembea Naye na Yeye Mungu akitembea nasi

Hii inakuja katika mvuto wa tatu! inaamini ni hilo. Ninatendea kazi kitu fulani; inachukuwa kiasi hiki cha Imani na kurudi hadi nyuma na kuanza na kuja katika hali ya kuinua Imani ndani iliyo fungiwa kwenye mabano hali ambayo hujawahi ona kwa njia hiyo kabla . sio Imani hii, bali Imani kamilifu.

Uijenge hiyo ndani ya moyo wako. Na umuangalie Mungu mkamilifu, na moyo mkamilifu, kwa Neno kamilifu ambalo ni kali kuliko upanga ukatao kuwili ambalo lina uwezo wa kupambanua siri za mioyo (Waebrania 4:12-13) ni nini? tuna

kuja sasa katika ule ukamilifu, kwa sababu watu inabidi walifikie hilo kwa ajili ya ule unyakuo.

Hicho ndicho kinauzuia usitokee hivi sasa mpaka hilo Kanisa lifikie kwenye Imani kamilifu ya kunyakuliwa. Ninaitafuta hiyo.

Kwangu inamaanisha kujitikisa kwingi. inamaanisha mengi kwenu; lakini kwa pamoja tutafanikiwa kwa neema ya Mungu.Amen. [ 1 ]

Nukuu za kiingerez\
[1] Imani Kamilifu(63-0825) Aya39, 26,19-20, 51 – 77 , 93 -94, 112 – 114, 123 – 134, 184.
[2] Maji yadumuyo kutoka katika Mwamba (61 -0723M) Aya 147,150-153, 160
[3] Kimo cha mtu mkamilifu (62-1014M) uk.33

---

Jiwe la kujengea la kiroho nambari 189 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa saa hii, yamekusanywa na Gerd rodewald friendestr. 69.D-75328 Schomberge Germany Simu (+49) 2357613 Fax 72353306.

---

Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Bibilia na kazi ya haraka itazunguka dunia.Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo, utaratibu na mafundisho uk724.)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa:

*Charles E. Y. Kanju,*

*Box 553 Korogwe - Tanga*

*E-mail: Chaelika@livel.com*

*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*